**Unaweza Kusikia Sauti ya Mungu!** Na Mark Virkler

Nilijitupa na kugeuka kitandani, nikashindwa kulala. Wazo liliendelea kuwepo akilini mwangu: “Je! Ikiwa ningekufa usiku wa leo? Siko tayari kwenda mbinguni." Kwa kuwa sikuweza kuliondoa hilo wazo, niliinuka, nikashuka chini ya ghorofa na nikasubiri wazazi wangu warudi nyumbani kutoka mkutanoni kwao. Walipofika, nilitangaza kwamba ninataka kuokoka, na walinipeleka moja kwa moja nyumbani kwa mchungaji ambapo alielezea mpango wa wokovu na kuniongoza katika sala ya toba ya mwenye dhambi. Nilikuwa na miaka 15 wakati nilimkubali Yesu Kristo ndani ya moyo wangu kama Bwana na Mwokozi wangu.

Ilikuwa sauti ya Mungu ambayo ilikuwa ikiongea nami usiku huo, ikiniita kuingia kwenye ufalme Wake. Sauti yake ilikuja kama mawazo huria ndani ya kichwa changu. Hata hivyo, sikutafsiri hii kama njia ya msingi ya sauti ya Mungu kusikika hadi nilipomaliza mahangaiko ya miaka 10 ya utafutaji wa kusikia waziwazi wa sauti ya yake.

Ukristo ni wa kipekee kati ya dini, kwa sababu unajenga uhusiano wa kibinafsi na Muumba kuanzia hapa na sasa, na wa kudumu milele. Yesu alisema, "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli" (Yohana 17:3). Kwa bahati mbaya, wengi Kanisani wanakosa baraka kubwa ya ushirika na Bwana wetu kwa sababu tumepoteza uwezo wa kutambua sauti yake. Ingawa Yohana 10:27 inatuahidi kwamba "Kondoo wangu waisikia sauti yangu," waamini wengi sana wanaona njaa ya uhusiano huo wa karibu ambao pekee ndio unaoweza kutosheleza hamu ya mioyo yao.

Nilikuwa mmoja wa wale kondoo ambao hawakuweza kutambua sauti ya Mchungaji wangu. Nilitamani uhusiano wa ukaribu zaidi wa kiroho na Mungu, lakini sikuweza kuupata. Kisha katika mwaka wa kumi na moja wa maisha yangu ya Kikristo nilipa mawazo huria ya kwamba "nilipaswa kutenga mwaka wa maisha yangu wa kujikita katika kujifunza kusikia sauti ya Mungu." Niliamua kufanyia kazi wazo hilo na kujishughulisha kujifunza kusikia sauti yake. Sikujua, ilikuwa ni Bwana akiniita niwekeze wakati huo.

Mwaka huo Bwana alifunua funguo nne rahisi, zote zinapatikana katika Habakuki 2:1, 2, ambapo ilifungua hazina ya sauti yake. Kwa kutumia funguo nne kwa pamoja kuliniruhusu kusikia kwa urahisi sauti ya Mungu kila siku. Ilikuwa hatua iliyonibadilisha zaidi katika miaka 45 ya maisha yangu ya Kikristo! Ningependa kukushirikisha na wewe ili uweze kuzijaribu na uone ikiwa zinafanya vivyo hivyo kwako.

**Ufunguo: Sauti ya Mungu moyoni mwako mara nyingi inasikika kama mtiririko wa mawazo huria.**

Habakuki alijua sauti ya Mungu iliyokuwa ikizungumza naye (Hab. 2:2). Eliya aliielezea kama sauti ndogo,ya utulivu (1 Wafalme 19:12). Siku zote nilikuwa nikisikiliza sauti ya ndani yenye kusikika, na Mungu huongea hivyo wakati mwingine. Hata hivyo, niligundua kwa kawaida, sauti ya Mungu huja kama mawazo huria, au mtiririko wa mawazo.

Kwa mfano, je! Haujawahi kuendesha gari barabarani na wazo likaja kwako kumwombea mtu fulani? Je! Hauamini kuwa ni Mungu alikuambia uombe? Sauti ya Mungu ilisikika kama nini? Ilikuwa ni sauti inayosikika, au ni mawazo huria ambayo hutoa mwanga akilini mwako?

Uzoefu unaonyesha kuwa tunatambua mawasiliano ya ngzai ya kiroho kama mawazo huria, hisia na maono, na Maandiko yanathibitisha hii kwa njia nyingi. Kwa mfano, tafsiri moja wapo ya paga, neno la Kiebrania la maombezi, ni "tukio la kukutana au kukutana kibahati." Mungu anapoweka jambo mioyoni mwetu, Yeye hufanya hivyo kupitia paga, kukutana na akili zetu "kwa bahati". Tunachukulia kukutana kwa bahati kwa kuwa hatukufikiria juu ya wazo husika, hata hivyo lina kusudi, kwa sababu Mungu ndiye aliyelituma wazo hilo.

Kwa hivyo, unapotaka kusikia sauti ya sssMungu, unajielekeza kwenye kukutana kwa mawazo kwa bahati, mawazo huria au mtiririko wa mawazo. Hata mawazo ya Shetani yanakuja kwetu kama mawazo huria, ndiyo maana tumeamuriwa "kuanguasha mawazo" (2 Wakorintho 10:5). Nina hakika sote tumewahi pata mawazo mabaya, hata yakishambulia wakati wa maombi na kuabudu. Kwa hivyo ninahitimisha kuwa mawazo ya uchambuzi ni yangu, mawazo huria mazuri hutoka kwa Roho Mtakatifu, na mawazo huria mabaya hutoka kwa roho chafu.

- **Mawazo ya Mungu:** yanaambatana na maandiko na majina yake mbali mbali: Mfariji, Mshauri, Mwalimu, Mtoaji wa Uzima, Mponyaji na Mkombozi. Mawazo yake hujenga, kuhimiza, na faraja. Ni safi, yenye amani, upole, yenye busara, yamejaa rehema na matunda mazuri, thabiti (Yakobo 3:17).
- **Mawazo ya Shetani:** yanaambatana na majina yake: mshtaki, adui, mwizi anayekuja kuua, kuiba na kuharibu. Mawazo yake huhukumu na kuleta kukata tamaa, kukataliwa, hofu, shaka, kutoamini na kwa jumla, shida. Mawazo ya Shetani huleta wivu na tamaa ya ubinafsi (Yakobo 3: 14,15).

**Ufunguo: Tulia ili upambanue mtiririko wa mawazo ya Mungu**

Habakuki alisema, "Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara ..." (Habakuki 2:1). Habakuki alijua ya kusikia mawazo ya Mungu tulivu, ya ndani na huria, lazima kwanza aende mahali tulivu na kutuliza mawazo yake na hisia zake. Zaburi 62:5 inatutia moyo tumgoje Mungu kwa kimya. Kuna ufahamu wa ndani wa ndani (mtiririko huria) katika roho zetu ambao kila mmoja wetu anaweza kupata wakati tunanyamazisha miili yetu na akili zetu. Ikiwa hatuko na utulivu, tutahisi mawazo yetu tu.

Kumpenda Mungu kupitia wimbo wa ibada ya utulivu ni njia moja nzuri ya kutulia. (Kumbuka 2 Wafalme 3:15.) Baada ya mimi kuabudu na kunyamaza ndani, najielekeza kwenye mtiririko huo huria. Ikiwa mawazo yanakuja juu ya vitu ambavyo nimesahau kufanya, ninaandika ili niweze kufanya jambo hilo baadaye. Ikiwa mawazo ya hatia au kutojithamini yanakuja, ninatubu kwa thati, na ninapokea kuoshwa kwa damu ya Mwanakondoo, na ninavaa vazi lake la haki, najiona sina doa mbele ya Mungu (Isaya 62: 10; Wakolosai 1: 22).

**Kuwa na lengo dhahiri husababisha mtiririko safi kabisa:** Kupokea neno safi la Mungu, ni muhimu sana kwamba moyo wangu uwe umejielekeza kwa usahihi wakati ninakaa kimya kwa sababu mtiririko wa hisia za ufahamu hutokana na kinachoonekana mbele ya macho ya mtu. Ikiwa nitamtazama Yesu, mtiririko wa hisia za ufahamu zinakuwa safi na hutoka kwa Yesu. Lakini ikiwa nitaangalia kwa macho yangu juu ya hamu fulani ya moyo wangu, mtiririko wa hisia za ufahamu huathiriwa na hamu hiyo. Ili kuwa na mtiririko safi lazima niwe kimya na kwa uangalifu kumtazama Yesu (Waebrania 12:2).

Tena, kumwabudu Mfalme kimya kimya, na kupokea ukiwa katika utulivu ambao unafuatia hapo hukamilisha hili. Naanza wakati wangu wa maombi kama vile Yesu alivyotufundisha kusali ni muhimu: "Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe ..." Yesu alitufundisha kuanza maombi kwa kuinua macho yetu juu kwa Baba yetu tukimtazama. Hatuanzi maombi na masuala yetu. Tunaanza sala yetu kwa kumtazama!

**Ufunguo: Tukimtazama Yesu na Kupokea Maono**

Habakuki alisema, "nitaangalia ili nione," (Habakuki 2:1,2). Kwa kweli Habakuki alikuwa akitafuta maono alipokuwa akiomba. Kwa kuwa ninaamini Bibilia imekusudiwa kuiishi, niliamua kwamba mimi pia, nitaanza kutazama kwa macho ya moyo wangu kuingia kwenye ulimwengu wa Roho ili kuona kile ninachoweza kuona.

Fanya kile Mfalme Daudi alifanya! Njia nzuri ya kuanza kutumia macho ya moyo yako ni kufanya yale ambayo Mfalme Daudi alifanya: "Maana Daudi ataja habari zake, NALIMWONA BWANA MBELE YANGU SIKU ZOTE, KWA KUWA YUKO UPANDE WA MKONO WANGU WA KUUME, NISITIKISIKE."(Matendo 2:25). Zaburi ya mwanzo inaweka wazi kuwa huu ulikuwa uamuzi wa Daudi, haikuwa kutembelewa daima kiungu:"**Nimemweka** Bwana mbele yangu daima, Kwa kuwa yuko kuumeni kwangu, sitaondoshwa. "(Zaburi 16:8). Kwa sababu Daudi alijua kuwa Bwana alikuwa pamoja naye kila wakati, aliamua katika roho yake kuona ukweli huo kwa macho ya moyo wake katika maisha. Akijua kwamba hii ingefanya imani yake kuwa na nguvu.

Tunasema, "Picha inafaa kuliko maneno 1000." Ninaamini hiyo ni kwa sababu picha ni lugha ya moyo. Tunaona kuwa Yesu alitumia picha kila wakati alipofundisha (Mathayo 13:34). Ninapotumia picha katika wakati wangu wa maombi, kuweka macho yangu kwa Yesu, ninazungumza lugha ya moyo wangu na ambayo inanipeleka haraka ndani ya ukweli wa moyo / roho inifikisha kwenye zaidi ya akili yangu.

**Tumia fikra za Kimungu:** Kwa hivyo mimi huchagua kufanya kile Mfalme Daudi alifanya na ninakua na "fikra za kimungu," ambayo mimi hutafsiri kuwa "kuwa na picha kwenye fikra ya mambo ambavyo Mungu asemavyo." Ni wazi ikiwa picha kwenye fikra zangu kuwa Yesu hayuko nami, hiyo itakuwa ni uongo, ambayo sio busara. Siwezi kufikiria sababu yoyote ambayo ningependa kupiga picha kwenye mawazo ya vitu visivyo vya Kimaandiko. Kwa hivyo namuona Yesu mkono wangu wa kulia, siku zote. Ninaongeza hili kwenye maombi ya Paulo kwa Mungu, macho ya moyo yatiwe nuru (Waefeso 1:17,18).

Halafu najielekeza kwenye mtiririko wa Roho Mtakatifu, na Yeye huhuisha picha nizionazo. Najikuta naweza kutoka kwenye picha kwenye fikra ya kimungu, na kuwa maono ya Kimungu.

Inashangaza, ni rahisi na kama kitoto! Kwa kweli inahitajika kuwa hivyo, kwani tunaambiwa kwamba ili tuingie katika ufalme lazima tuwe kama watoto wadogo. Mjukuu wangu wa miaka 6 anaweza kufanya hivi na hunishirikisha maongezi yake na Mungu na maono ya malaika wakisimama pande zote zake wakimlinda na kumtunza. Utagundua kuwa watoto wako wadogo wanaweza kutumia funguo hizi nne kwa urahisi kuliko unavyoweza! Jaribu pamoja nao na uone.

Kuanzia kitabu cha Mwanzo hadi Ufunuo Mungu alitoa ndoto na maono, na alisema kimahususi kwamba katika siku za mwisho atamwaga Roho wake na tutaona ndoto na maono (Matendo 2:1-4,17).

Lazima tuangalie ikiwa tunataka kuona! Daniel aliona maono katika kichwa chake au mawazoni mwake akasema, "Katika maono yangu usiku nilitazama ... Nilipoendelea kutazama ... nilitazama" (Daniel 7:2,9,13 NEN). Kwa hivyo nilihitaji kutubu kwa kutotazama, na kuanza kuyatoa kwa Bwana macho ya moyo wangu, na kutazama. Ninapoomba, ninamtazama Yesu, na ninatazama na kusikiliza wakati anaongea nami, nami hufanya vilivyopo moyoni mwake. Wakristo wengi wataona kuwa ikiwa wataangalia tu, wataona picha zikitiririka, kwa namna ile ile wanapokea mtiririko wa mawazo.

Yesu ni Immanueli, Mungu pamoja nasi (Mathayo 1:23). Ni rahisi namna hiyo. Unaweza kumuona Kristo yuko pamoja nawe kwa sababu Kristo **yuko** pamoja nawe. Kwa kweli, maono yanaweza kuja kwa urahisi sana kwamba utajaribiwa kuyakataa, ukidhani kuwa yanatokana nawe tu. Lakini ikiwa utaendelea kuzirekodi picha hizi zinazotiririka ndani yako, mashaka yako yatashindwa na imani wakati utakapogundua kuwa yaliyomo ndani yake yaweza kuzaliwa na Mungu Mwenyezi.

**Namna ya kuishi:** Yesu alionesha uwezo wa kuishi daima akiwasiliana na Mungu, akitangaza kuwa hakufanya chochote kwa kuanzisha yeye, ila tu kile *alichomuona Baba akifanya, na kumsikia Baba akisema (Yohana 5: 19,20,30) ). Njia bora sana ya kuishi!*

Je! Inawezekana kwako kuishi kwa kile tu kinachotokana na Mungu kama Yesu? Ndio! Inaitwa "kukaa ndani ya Kristo" (Yohan 15). Mtazame Yesu. Pazia limepasuka, likitupa uwezo wa kumfikia Mungu wa karibu, na Yeye anakuita mkaribie (Luka 23:45; Waebrania 10:19-22). "Ninaomba macho ya moyo wako yatiwe nuru" na utaona maono yake. Ni zawadi yake kwako, itolewayo bure (Matendo 2:17).

**Ufunguo: Kuandika, yaani andika maombi yako na majibu ya Mungu, huleta uhuru mkubwa katika kusikia sauti ya Mungu.**

Mungu alimwambia Habakuki aandike maono hayo (Habakuki 2:2). Hii haikuwa amri ya pekee. Maandiko yanaandika mifano mingi ya maombi ya mtu binafsi na majibu ya Mungu (mfano Zaburi, manabii wengi, Ufunuo).

Ninaita mchakato huo "kuandika yatokayo pande mbili," na nimeona kuwa kichocheo cha kushangaza kwa kutambua wazi mtiririko wa Mungu ndani yangu, mtiririko huria, kwa sababu kadiri ninavyoandika ninaweza **kuandika kwa imani** kwa muda mrefu, kwa kuamini kuwa ni Mungu. Ninajua kuwa kile ninaamini nimepokea kutoka kwa Mungu lazima kijaribiwe. Hata hivyo, kujaribu kunajumuisha mashaka, na mashaka huzuia mawasiliano na Mungu, kwa hiyo sitaki kupima wakati huo huo ninapokea (Waebrania 11:6). Kwa kuandika, naweza kupokea kwa imani, nikijua kuwa mtiririko utakapomalizika naweza kuujaribu na kuchunguza kwa umakini, kuhakikisha kuwa unaambatana na Maandiko (1 Wathesalonike 5:21).

**Ondoa shaka:** Mashaka yanaweza kukuzuia mwanzoni, lakini tupilie mbali, ujikumbushe kwamba kurekodi maneno na maono ya Mungu ni jambo la kibibilia, na kwamba Mungu yuko, akizungumza na watoto wake. Kwenye bibilia, Shetani huwa akitoa shaka kwa kusema, "Ati kweli Mungu alisema ...?" (Mwa. 3:1 NEN).

Jifunze kutulia! Tunapoacha masumbufu na kuingia katika pumziko lake, Mungu yuko huru kutiririka (Waebrania 4:10). Kaa kwa raha, chukua kalamu yako na karatasi (au kompyuta au iPad), tabasamu, na uelekeze mawazo yako kwa Bwana kwa sifa na kuabudu, ukitafuta uso Wake. Andika, "Habari za asubuhi, Bwana! Nakupenda. Unataka kuniambia nini?" Basi tulia kimya, ukimtazama Yesu. Utakuwa na wazo nzuri sana ghafla. Usiwe na shaka; liandike tu. Baadaye, utakaposoma uliyoandika, utabarikiwa kugundua kuwa yaliyomo ni ya kushangaza na kwamba kweli una mazungumzo na Mungu!

---

**Msikie Mungu kupitia kutiwa nuru kwa Maandiko:** Kumjua Mungu kupitia Bibilia ni msingi muhimu wa kusikia sauti yake moyoni mwako, kwa hivyo lazima uwe na dhamira dhabiti ya kujua na kutii Neno la Mungu lililoandikwa. Tumeamriwa kutafakari maandiko (Yoshua 1:8). Tunapoomba juu ya maandiko, tunapata mistari ambayo huhuishwa kwenye ukurasa huo na kutugonga katika macho. Hii ni njia nyingine ya nguvu sana ambayo Mungu husema nasi. Kutafakari maandiko mara kwa mara kunaamriwa na Mungu na ni lazima kwa maisha bora ya Kikristo.

**Tumia washauri wa kiroho:** Ni muhimu pia kwa ukuaji wako na usalama kuwa unahusiana na washauri madhubuti wa kiroho. Hoja zote kuu za mwelekeo ambazo zinakuja kwenye mazungumzo unayoandika zinapaswa kudhibitishwa na washauri wako kabla ya kuchukua hatua yoyote. Bibilia inasema kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno litathibitishwa (2 Wakorintho 13:1). Pia, katika wingi wa washauri, kuna usalama (Mithali 15:22). Kwa hiyo hakikisha unatembea kwa unyenyekevu na utafute na kupokea maoni kutoka kwa washauri wako wa kiroho. Hatua hii haipaswi kurukwa!

**Funguo hizi nne zinaonekana tena katika Ufunuo:** Yohana alitumia funguo nne kama alizotumia Habakuki. Katika Ufunuo 1:9-11 tunaona alikuwa katika roho (utulivu), akasikia sauti nyuma yake (alijielekeza kwenye uhuria), ikisema, "Andika katika kitabu (kuandika), unachokiona (maono)." Kwa

hivyo katika Agano la Kale na Jipya tunapata funguo nne zinazofanana zinatumiwa kupokea sauti ya Mungu. Usijali kuhusu mpangilio wa funguo. Hakikisha tu unatumia funguo zote nne.

**Kama KIFURUSHI hizi funguo nne (Tulia! Angalia! Sikiliza! Andika!)**: Huifanya kazi! Watu husikia. Tunakuhakikishia kwamba ikiwa utatumia funguo hizi nne **kwa pamoja**, zitafanya kazi na utasikia sauti ya Mungu. Jaribu kutumia kama kifurushi, na uone jinsi zinavyofanya kazi. Tunao muziki wa bure wa kupakua ambao unaweza kusikiliza unapoandika mazungumzo yako na Mungu. Unapatikana kwa www.cwgministries.org/galilee. Sehemu ya kwanza ya rekodi inakusaidia wewe kwenye safari ya maono na Yesu kando ya Bahari ya Galilaya, na kukuongoza katika kutumia funguo zote nne kwa pamoja. Tunakutia moyo ujaribu! Naomba urudishwe kwa kutembea na Bwana kwenye bustani wakati wa mchana uliotulia. Na uweze kuona utimilifu wa uhusiano wa kibinafsi na Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Ushirika na Mungu uwe wa undani katika maisha yako, na uponyaji wake na miale ya ubunifu ikujaze na kukushindia.